

Kikundi cha umri

16-24

Ndoa za

Utotoni



Ndoa za Utotoni ni nini?

Ndoa za utotoni ni pale msichana au mvulana wanapoingia katika ndoa wakiwa chini ya umri wa miaka 18. Kwa kawaida, ndoa hiyo huwa kati ya msichana na mwanaumwe aliyemzidi umri. Yaweza pia kuwa ndoa kati ya msichana na mvulana.

Kwa nini hili hutokea?

Zipo sababu nyingi zinazopelekea baadhi ya wanaume wenye umri mkubwa kutaka kuoja wasichana. Mara nyingi ni juu ya mila na tamaduni, na mawazo ya kizamani juu ya wanawake na wanaume.

Wakati mwingine, wasichana huolewa kwa kuwa wamepata mimba, au kwa sababu ya shinikizo kutoka kwenye familia kuwataka waolewe kabla hawajapata mimba.

Wazazi pia wanaweza kuweka shinikizo kwa vijana kuingia katika ndoa kutokana na mila, au kwa vile wao ni maskini.

Je kuna Ubaya gani katika Ndoa za Utotoni?

Ndoa za Utotoni huathiri afya ya msichana, elimu, Usalama, na furaha. Wasichana waolewapo wakiwa chini ya umri, ina maana:

- ▲ **Wasichana huacha kwenda shule.** Bila elimu nzuri, wasichana hawawezi kupata kazi nzuri itakayomuwezesha kuendesha maisha.
- ▲ **Wasichana hupata mimba wakiwa katika umri mdogo,** kabla miili yao kuwa tayari. Hii huongeza hatari matatizo ya hatari, maradhi na hata kifo.

- ▲ **Wasichana wapo katika hataari zaidi ya kupata VVU** na magojwa yatokanayo na ngono, kwa kuwa hawajajengeka kikamilifu.
- ▲ **Wasichana wana hatatari ya kufanyiwa ukatili** kihisia, na kimaumbile kutokana na nguvu za kimahusiano zisizolingana kati ya msichana na mwanaume.
- ▲ **Wasichana hujikuta wamekatwa/wametengwa toka kwenye familia zao**, na marafiki zao ambao wapo bado shuleni.

Wasichana wanaoolewa katika umri mdogo, hawako huru kufanya maamuzi yao wenyewe, Wana majukumu mengi katika umri mdogo ikiwemo kuwa mama, kutekeleza majukumu ya nyumbani na kuwahudumia waume zao, pia hawana mda wala uhuru wa kujiangalia wao wenyewe au kupanga mambo ya baadaye.

Ndoa za Utotoni huwadhulumu wasichana utoto wao, na ndoto zao za baadae. Bali kuchelewa kuolewa kwa msichana hadi kufikia utayari, kunamwezesha kuweza kufanya maamuzi yake katika maisha.

Tunawezaje kutokomeza Ndoa za Utotoni ?

Hakuna njia rahisi ya kutokomeza ndoa za utotoni. Watu wazima na vijana ni lazima tufanye kazi kwa pamoja.

Vijana wafanye eneo lao. Wewe na marafiki zako mnaweza kuleta mabadiliko kwa kusaidia kubadili mitazamo na imani ndani ya jamii yako. Ziko njia nyingi unazoweza kufannya, pamoja na:

- ✓ **Paaza sauti** Katika jamii yako dhidi ya Ndoa za Utotoni. Endapo wasichana watabaki mashuleni, basi huenda

wakaolewa baadae, watakuwa wenye afya na salama, na kupata kipato. Hii ni faida kwa wasichana, familia zao, na jamii – kila mtu!

- ✓ **Kuwathamini wasichana**, na kuelewa kuwa wao wana haki ya kufanya maamuzi juu ya maisha yao. Hii ina maana kuwa – kama ilivyo kwa wanaume na wavulana – wasichana wanaweza kuchagua kama ni kuolewa, na nani, au lini. Wanayo haki kuamua nani wa kufanya nae ngono, wawe na watoto wangapi, na kwa wakati gani. Pia wasichana wana haki kufanya ngono salama: kutumia kondom kujikinga na magonjwa yatokanayo na ngono, ikiwa ni pamoja na UKIMWI.
- ✓ **Kutoa taarifa**, kwa walimu wenu, wazazi, na viongozi katika jamii, endapo imeonekana msichana analazimishwa kuolewa.
- ✓ **Kuwakumbusha** watu wanao walazimisha wasichana kuolewa, kuwa wanavunja sheria, na sheria itachukua mkondo wake dhidi yao.

Watu wazima ambao wanataka kutokomeza ndoa za utotoni, wameweza kubadili sheria katika nchi nyingi na kulifanya suala la ndoa za utotoni kuwa ni kosa la jinai. Wanashirikiana na vijana kuhakikisha kuwa sauti za wasichana na wavulana zinasikika pale maamuzi muhimu yanapofanyika, kama vile kubadilisha sheria na sera. Jisomee juu ya juhudi hizo hapa: